Usomaji wa Majibizano: Kuwa na Mazungumzo Kuhusu Vitabu

Na Jessica Sidler Folsom, Ph.D.
Assistant Research Scientist, Kituo cha Utafiti wa Kusoma Iowa

Wazazi na Walimu wote karibu ulimwengu wote wanakubali umuhimu wa kusoma kwa watoto. Hata waganga wa watoto na hospitali wanahamasisha hilo. Hata hivyo, kusoma kwa sauti kunaweza kuwa na thamani kubwa kielimu kuliko kufanywa kama shughuli ya nyongeza kabla ya kulala au chakula cha mchana.

Ni rahisi tu kuchukua kitabu kwenye kabati, kukisoma, na hata kuuliza maswali machache mwishoni mwa hadithi bila kufikiria zaidi juu ya uchaguzi wa kitabu au dhumuni la kusoma hiyo hadithi. Pengine ni kipendeleo cha mtoto, au ina urefu unaostahiki wa muda uliopangwa. Pengine inafaa kwa mada ya wiki ya darasa. Hata hivyo, hii ni mifano inayotolewa na wakubwa. Mkubwa anachagua kitabu, anasoma hadithi, na kuuliza maswali au kuongoza mjadala.

Njia mbadala ya kuhusisha zaidi au yenye manufaa zaidi ni usomaji wa kuingiliana au usomaji wa majibizano. Usomaji wa majibizano huhusisha mkubwa na mtoto kwa majibizano kuhusisiana na maelezo wanayosoma. Mazungumzo yao yanahusisha kutafsiri misamiati mipya, kuboresha umahiri katika kuongea, kutambulisha sehemu za hadithi, na kutengeneza ujuzi wa masimulizi.

Wakati wazazi na walimu wanapopanga na kutekeleza usomaji wa majibizano, utafiti unapendekeza inaweza hasa kufaa katika kuboresha ujuzi kama vile uelewa wa maandishi, lugha ya kuzungumza, na uwezo wa kufahamu. Muhimu zaidi, husaidia kutengeneza namna gani msomaji mzuri anafikiri kuhusu maandishi anapokuwa anasoma. Faida ya usomaji wa majibizano siyo tu kwaajili ya watoto. Ingawa dhima alianzia kwa usomaji wa vitabu vya picha kwa watoto ambao hawajaanza shule (Whitehurst et al., 1988), sehemu kubwa ya utafiti imeongeza matumizi yake kwa watu wa umri mwingine na umma wakiwemo wanafunzi wenye ulemavu (What Works Clearinghouse, 2010), wanaosoma kwa shida (Swanson et al., 2011),na wanaojifunza Lugha ya Kiingereza (Brannon & Dauksas, 2014).

©IOWA READING RESEARCH CENTER 2017

Viwango tofauti vya Maswali kwenye Usomaji wa Majibizano

Utekelezaji wa kitamaduni wa usomaji wa majibizano huhusisha kusoma kwa kurudiarudia kitabu hicho hicho na kujadiliana kuhusu viwango vitatu vya maswali (Flynn, 2011).

- **Maswali ya Kiwango cha 1** ni ya msingi aina ya maswali ya “wh” yakilenga kwenye kitu gani kinaweza kuonekana haraka (au kusoma) kwenye maandishi. Hatua ya 1 pia inahusisha utambulishaji wa msamiati mpya. Kwa mfano, wakati wa kuonyesha picha, msomaji mkubwa anaweza kuuliza “Aina gani ya miguu mnyama huyu anayo?” Hapa mkubwa anatafuta jibu sahihi na mahususi ilii kuongeza misamiati ya kuongea kwa mtoto.
- **Maswali ya Kiwango cha 2** ni ya wazi na yanatumika kupata mrejesho wa mtoto. Kwa mfano, msomaji mkubwa lazima aulize, “Kitu gani kinatokea kwenye sehemu hii ya hadithi?” Hapa mkubwa anajaribu kumtia moyo mtoto kushirikisha kile ambacho mtoto anafikiri kuhusu na kutengeneza maana kutoka kwenye maelezo.
- **Maswali ya Kiwango cha 3** ni ya kiwango cha juu zaidi na kutambulisha dhana kama sehemu za maelezo na sehemu za hadithi. Kwa mfano, msomaji mkubwa anaweza kuuliza, “Mhusika mkuu alikuwa nani na alijisikiaje? Hii pia inaweza kujumuisha maswali ambayo yanamtenganisha mwanafunzi na maelezo na kuunganisha hadithi na maisha yao binafsi. Kwa mfano, “Ungejisikiaje kama hicho kingetokea kwako?”

Tofauti Kati ya Njia Sahihi na Zisizo sahihi za Kutumia Usomaji wa Majibizano

Usomaji wa Majibizano...

- **Siyo** "mwalimu anasoma, wanafunzi wanasikiliza"
- **Siyo unaongozwa na walimu**
- **Hauna ukomo** katika kusimulia maelezo yenye maswali na majadiliano mwishoni
- **Siyo tu** kwa watoto wadogo

Usomaji wa Majibizano...

- **Ni** wa muingiliano
- **Unamlenga** mwanafunzi
- **Unaendeshwa** kwa simulizi yenye maswali na majadiliano muda wote.
- **Ni** shughuli inayohitaji upangiliaji mzuri
- **Ni** kwa ajili ya wanafunzi wa ngazi zote

Ingawa mbinu mbalimbali zipo kuwezesha maswali matatu katika usomaji wa majibizano, mbinu mbili maarufu zinajulikana kwa kifupi CROWD na PEER. Zote zimezungumziwa kwenye taarifa za blogu ya IRRC, na taarifa hii itaongezea kwenye mbinu mbili na kutoa nyenzo nyingine ili kusaidia kupangilia shughuli ya usomaji wa majibizano.

Kutosheleza Madaraja Mbalimbali ya Swali na CROWD

CROWD inatumika kukumbuka aina ya maswali ya kuuliza:
Kumalizia, kukumbuka, yaliyowazi, maswali ya "**w**h", na kutengenisha. Nyongeza ya CROWD ni CROWD-HS, ambayo hutumika kuhamasisha kutenganisha kwa wakati kunakohusiana na nyumbani na shule. Hapa ni mfano wa maswali ya CROWD-HS kwaajili ya hadithi inayofahamika vizuri *Nguruwe Wadogo Watatu*.

Swali la kumalizia: "nitapumua kwa nguvu, na nitahema kwa nguvu, na nita_____ _____ _____ _____."

Jibu: Piga nyumba yako chini.

Swali la kukumbuka: Nyumba ipi ambayo Mmbwa Mwitu Mkubwa hakuweza kuipiga?

Jibu: Iliyojengwa na matofali.

Swali lililowazi: Kwanini unafikiri nguruwe wa kwanza alijenga nyumba yake kwa kutumia mabua?

Jibu: Ilikuwa rahisi kujenga. Alikuwa mvivu.

Swali la "**W**h": Aina gani ya mnyama alikuwa akiwafukuzia nguruwe?
Jibu: Mbwa mwitu.

Kutenganisha: Unafikiri nguruwe walijisikiaje wakati mbwa mwitu alipojaribu kuwafikia?

Jibu: (majibu yatatofautiana.) Waliogopa, hasira, uchungu.

Swali la nyumbani: Kama ungetakiwa kujenga nyumba ya kuchezea nyumbani, ungejenga ya aina gani?

Jibu: (Majibu yatatifautiana.) Nyumba ya miti, turubai, boma.

Swali la shule: Mbwa mwitu alikuwa na amri. Alikuwa anamaanisha kwa watoto watatu wa nguruwe. Utafanyaje iwapo mtu anakuamrisha shuleni?

Jibu: (Majibu yatatofautiana.) Nitamwambia mwalimu. Nitawaambia waache. Nitawapuuza.

Hamasisha Majibizano zaidi na PEER+PA

CROWD-HS inasaidia kukumbuka aina za maswali ya kuuliza, lakini kumbuka kwamba lengo ni kuchochea majibizano kuhusu hadithi, na siyo majibu ya haraka ya neno moja. Mbinu ya PEER (**H**araka**, T**athmini, **O**ngeza, na **R**udia) inaweza kutumika kusaidia mkubwa kuhamasisha majibu ya kina. Nyongeza ya PEER ni PEER+PA, ambayo hutumika kukumkumbusha mkubwa kumsifia mtoto kwa kushiriki kwenye mazungumzo na kusaidia kutumia majibu ili yawe na maana. Sehemu hizi zinatumika wakati wote wa majibizano na mtoto. Hapa ni mfano wa kutumia PEER+PA yenye moja ya maswali ya hapo juu ya CROWD-HS:

Bila kuchelewa mtoto aseme kitu kuhusiana na kitabu.

Mkubwa: Aina gani ya mnyama alikuwa akiwafukuzia nguruwe wadogo?
Mtoto: Mbwa mwitu.

Tathmini jibu la mtoto.

Mkubwa anafikiri mwenyewe, “Ndio, alikuwa mbwa mwitu, lakini tunaweza kuongeza zaidi kwenye hilo jibu.”

Panua jibu la mtoto.

Mkubwa: Ndio, alikuwa mbwa mwitu mkubwa, mbaya!

Rudia bila kuchelewa.

Mkubwa: Aina gani ya mnyama alikuwa akiwafukuzia nguruwe wadogo?
Mtoto: Mbwa mwitu mkubwa, mbaya!

Msifu na **T**umia jibu la mtoto.

Mkubwa: Hiyo ni sawa! Mbwa mwitu mkubwa mbaya alikuwa akiwafukuzia nguruwe wadogo. Kazi nzuri kukumbuka hadithi! Ungejisikiaje iwapo ungemuona mbwa mwitu mkubwa mbaya?
Mtoto: (Majibu yatatofautiana.) ningeogopa na kukimbia.

Ufundishaji wa Msamiati Kupitia Usomaji wa Majibizano

Kumbuka kwamba lengo muhimu la usomaji wa majibizano ni kuongeza au kupanua ujuzi wa lugha ya kuongea kwa wanafunzi , hasa msamiati. Njia moja ya kufanya hivi ni kujiingiza kwenye shughuli kabla ya kusoma ili kufundisha misamiati mikuu. Kama ilivyo kwamba kuna viwango vya maswali ili kuwezesha majibizano kuhusu maelezo, ni rahisi kufikiri kuhusu maneno ya msamiati kwenye madaraja haya matatu:

- **Maneno ya Daraja la 1** ni misamiati ya msingi ya maneno ambayo yanapaswa kuonekana na mtoto na mepesi. Maneno ya daraja la 1kwenye hadithi ya Nguruwe Wadogo Watatu yanajumuisha: nyumba, nguruwe, mbwa mwitu.
- **Maneno ya Daraja la 2** yanatokea mara kwa mara kwenye maelezo kwaajili ya watumiaji wazoefu wa lugha. Maneno haya yanaweza kuwa magumu kusaidia kuongeza kuonekana na misamiati myepesi kwa mtoto. Neno la Daraja la 2 kwenye hadithi ya Nguruwe Wadogo Watatu yanaweza kuwa mkubwa (baadhi ya matoleo ya hadithi yanabainisha nguruwe wa kwanza kama ndio mkubwa wa wa wale watutu).
- **Maneno ya Daraja la 3** ni miliki mahsusi na funzo bora pale inapohitajika kwenye eneo la yaliyomo au kwenye muktadha mahususi. Maneno haya hayatokei sana kwenye hadithi kama Nguruwe Wadogo Watatu. Hata hivyo, toleo gumu zaidi la hadithi linaweza kujumuisha neno la Daraja la 3 kwaajili ya kifaa cha uashi alichotumia nguruwe wa tatu: kikoleo.

Ingawa baadhi ya maneno yanaweza kutambulishwa wakati wa usomaji wa kujibizana, ni muhimu kuainisha kwa makini na kufundisha tena maneno yoyote ambayo yanaweza vinginenvyo kuingilia ufahamu wa kitabu wa mwanafunzi. Msomaji mkubwa anaweza kuainisha maneno ya Daraja la 2 ambayo yanatakuwa msaada kwa kuelewa maelezo ya sasa na kwamba mtoto anaelekea kuyatumia au kusoma kwenye mipangilio mingine.

Sasa kwamba tunaogelea kwenye supu ya viwango, madaraja, na herufi, tunawekaje vichwa vyetu juu ya maji, kuleta pamoja, na hasa kushiriki kwenye majibizano? Jambo la muhimu ni kuandaa kikamilifu! Hii inajumuisha kuchagua maelezo sahihi ambayo yanahamasisha majibizano, kubainisha misamiati ili kufundisha kabla, kufikiria kuhusu maswali ya CROWD-HS, na kutarajia majibu ya mtoto ambayo unaweza kutumia PEER+PA kupanua majibizano. **Mwongozo wa Kusoma kwa Kuingiliana** hapo chini unaweza kuwekwa kwenye kila kitabu ili kukusaidia kupanga msamiati na maswali utakayoyajumuisha. Maswali yanapaswa kuulizwa kwenye maelezo yote, siyo tu mwishoni, hivyo usisahau kuweka kumbukumbu ya namba ya karatasi kwa kila moja! Hii itakurahisishia wewe au mtu mwingine kuona malengo husika kwaajili ya kuanzisha mazungumzo anapotekeleza usomaji wa majibizano.

Alama/maingizo ya Kitabu kusaidia katika Usomaji wa Majibizano

Seti ya Vitabu Vitatu vya Mwongozo wa Usamaji wa Kuingiliana kwaajili ya Kupakua
Seti ya Alama za CROWD nne kwaajili ya Kupakua
Seti ya Alama za PEER nne kwaajili ya Kupakua

Marejeo

Brannon, D., & Dauksas, L. (2014). The effectiveness of dialogic reading in increasing English language learning preschool children's expressive language. *International Research in Early Childhood Education*, *5*, 1-10.

Flynn, K. S. (2011). Developing children's oral language skills through dialogic reading: Guidelines for implementation. *Teaching Exceptional Children*, *44*, 8-16. doi: 10.1177/004005991104400201

Stephenson, J. (2010). Book reading as an intervention context for children beginning to use graphic symbols for communication. *Journal of Developmental and Physical Disabilities*, *22*, 257-271. doi: 10.1007/s10882-009-9164-6

Swanson, E., Vaughn, S., Wanzek, J., Petscher, Y., Heckert, J., Cavanaugh, C., . . . Tackett, K. (2011). A synthesis of read-aloud interventions on early reading outcomes among preschool through third graders at risk for reading difficulties. *Journal of Learning Disabilities*, *44*, 258-275. doi: 10.1177/0022219410378444 | Full article

What Works Clearinghouse (2010). *What Works Clearinghouse intervention report early childhood education interventions for children with disabilities: Dialogic reading.* Washington, DC: Institute for Education Sciences. Retrieved from http://ies.ed.gov/ncee/wwc/InterventionReport/136

Whitehurst, G. J., Falco, F. L., Lonigan, C. J., Fischel, J. E., DeBaryshe, B. D., Valdez-Menchaca, M. C, & Caulfield, M. (1988). Accelerating language development through picture book reading. *Development Psychology*, *24*, 552-559. doi: 10.1037/0012-1649.24.4.552